TANGAZO LA SERIKALI Na. 206 la tarehe 17/3/2023

# SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

### MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (ADA NA USHURU) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI YA MWAKA 2023

Jina

TS Na 217 la tarehe 15/4/ 2022

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2023, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya Kifungu cha 8

2. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta na badala yake kukiandika upya Kifungu hicho ili kisomeke kama ifuatavyo:

"Muda wa kusafirisha mazao

8. Mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi itatakiwa kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni."

Dodoma,
Machi, 2023

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB.),
*Waziri wa Nchi – OR- TAMISEMI*